# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO (C.M.T.) KILICHOFANYIKA TAREHE 10/12/2021 KATIKA UKUMBI WA MANISPAA MUSOMA

**Mahudhurio**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1) Bosco O. Ndunguru | - MD | - | Mwenyekiti |
| 2) Lazaro N. Nangale | - Ag. MECON | - | Katibu |
| 3) Asteria Ruzangi | - MAICO | - | Mjumbe |
| 4) Jackson Godo | - DSQAO | - | Mjumbe |
| 5) Livingstone Kahwa | - MT | - | Mjumbe |
| 6) David J. Muharagi | - MHRO | - | Mjumbe |
| 7) Deus O. Nyakriga | - Ag. MELO | - | Mjumbe |
| 8) Bakari A. Sagini | - MEO (P) | - | Mjumbe |
| 9) Joseph Luhwa | - MFO | - | Mjumbe |
| 10) Reginard Kinyenje | - Ag. MPSO | - | Mjumbe |
| 11) Dr. Magreth Shaku | - Ag MMOH | - | Mjumbe |
| 12) Anicas Vilumba | - MTPO | - | Mjumbe |
| 13) Fikiri Kenyela | - MEMO | - | Mjumbe |
| 14) Recipicius Katundu | - MCDO | - | Mjumbe |
| 15) Johanes Kataraiya | - Ag. ME | - | Mjumbe |
| 16) Samwel Biyan | - K/TSC | - | Mjumbe |
| 17) Vicky Mbunde | - A/Tarafa | - | Mjumbe |
| 18) Mayenga Setta | - Ag. MLO | - | Mjumbe |
| 19) David L. Mboma | - RA | - | Mjumbe |
| 20) Nyachiti Tore | - Ag.MEO (P) | - | Mjumbe |
| 21) Ignatus S. Pauline | - Ag. MBO | - | Mjumbe |
| 22) Deogratius S. Lyimo | - Ag. MIA | - | Mjumbe |
| 23) Mafuru Mjarifu | - Ag. MPRO | - | Mjumbe |
| 24) Aines Anderson | - MLFO | - | Mjumbe |
| 25) Beatrice Marco | - M/TASAF | - | Mjumbe |
| 26) Charles Salyungu | - MTO) | - | Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA**

Hakuna.

**SEKRETARIETI**

1. Bahati Mugarula

**KUMB. NA. KWI/138/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa **7.43** mchana kwa kuwakaribisha wajumbe kushiriki kikamilifu katika kikao hicho

**KUMB. NA. KWI/1392021: KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zilizowasilishwa kikaoni na kukubaliwa kujadiliwa ni:-

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe **18/11/2021.**
4. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha tarehe **18/11/2021.**
5. Kupitia Muhtasari wa Kamati ya Fedha na Utawala cha tarehe **22/11/2021.**
6. Taarifa ya Mapato na Matumizi ya mwezi **Novemba, 2021.**
7. Taarifa ya Ununuzi na Ugavi ya mwezi **Novemba, 2021.**
8. Taarifa ya Mkataba wa kusafirisha nyaraka (EMS).
9. Taarifa ya ujenzi wa vyumba vya madarasa (UVICO -19) na ujenzi wa kituo cha Afya.
10. Taarifa ya uamuzi wa wazazi kuhusu uanzishwaji wa shule ya mfumo wa kiingereza (Mukendo).
11. Maombi ya mabadiliko ya matumizi ya fedha za ujenzi wa madarasa kutoka mapato ya Ndani pamoja na kuhamisha kifungu cha ujenzi wa shule mpya ya Kata ya Kigera.
12. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
13. Kufunga kikao.

**KUMB. NA. KWI/140/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 18/11/2021**

Muhtasari ulisomwa mbele ya wajumbe na kufanyiwa marekebisho na baadaye kuthibitishwa ili kuwa kumbukumbu halali za Halmashauri.

**KUMB. NA. KWI/141/2021: YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 18/11/2021**

Hapakuwepo na yatokanayo yaliyowasilishwa kikaoni.

**KUMB. NA. KWI/142/2021: KUPITIA MUHTASARI WA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI CHA TAREHE 22/11/2021**
Wajumbe walipitia Muhtasari wa Kamati ya Fedha na Utawala na kufanya marekebisho kwa ajili ya kuwasilishwa katika kamati husika

**KUMB. NA. KWI/143/2021: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWEZI NOVEMBA, 2021**
Mweka Hazina wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma aliwasilisha taarifa na kueleza kuwa, Halmashauri ilitegemea kukusanya na kutumia kiasi cha **Tshs. 23,251,693,466.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato kwa mwezi **Novemba, 2021** Halmashauri ilikusanya jumla ya **Tshs. 2,039,560,160.83** sawa na **asilimia 50.71** na kutumia jumla ya **Tshs. 1,608,804,135.00** sawa ma asilimia **21.21**. Aidha, alieleza kuwa, kufikia tarehe **30 Novemba, 2021** Halmashauri inadaiwa fidia ya viwanja kiasi cha **Tshs. 317,881,234.25**. Pia inadaiwa kiasi cha **Tshs. 640,112,372.99** na itaendelea kupunguza madeni hayo kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha

**Yatokanayo na taarifa hiyo.**

**Kuhusu hoja ya uchangiaji wa matumizi ya umeme na maji**

**Azimio.**
Maeneo yote yanayotumia umeme wa Halmashauri na maji yaainishwe kisha andiko liandikwe lipelekwe CMT kwa ajili ya kujadiliwa.

**KUMB. NA. KWI/144/2021: TAARIFA YA UNUNUZI NA UGAVI YA MWEZI NOVEMBA, 2021**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi aliwasilisha taarifa na kueleza kuwa shughuli zilizotekelezwa na kitengo cha Ununuzi na Ugavi kwa mwezi **Novemba, 2021** ni kama ifuatavyo:-
Vikao **2** vya kitengo cha usimamizi wa ununuzi na ugavi (PMU) na Bodi ya Zabuni. Alieleza kuwa kitengo kimeweza kufanya manunuzi yafuatayo kwa mwezi **Novemba, 2021.**

| | |
|---|---|
| (a) Vifaa na Bidhaa | Tshs. 37,866,997.72 |
| (b) Huduma zisizo za ushuri wa kitaalam | Tshs. 11,529,261.53 |
| **Jumla** | **Tshs. 49,396,259.25** |

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, waliijadili na kuipitisha

**_KUMB. NA. KWI/145/2021:_ TAARIFA YA MKATABA WA KUSAFIRISHA NYARAKA (EMS)**

Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi aliwasilisha taarifa na kueleza kuwa shirika la Posta Tanzania linafanya kazi ya kusafirisha vifurushi na nyaraka kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Aliendelea kueleza kuwa kutokana na uhitaji wa kuendelea kutoa huduma ya kusafirisha nyaraka za Halmashauri, Shirika limeona ni vyema kutoa huduma na kisha kulipa kwa bili na mkataba umefanyiwa mapitio na Halmashauri kupitia Kitengo cha Sheria.

Aliendelea kueleza kuwa maoni na marekebisho juu ya mkataba huo yawasilishwe ofisi ya Mwanasheria kabla ya kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala. Aidha alieleza kuwa kwa kuwa Halmashauri haikutenga bajeti hivyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023** kila Idara itenge bajeti ya kusafirisha nyaraka na vifurushi Menejimenti ilishauri usafirishaji wa vifurushi usimamiwe na Ofisi ya Utawala na Utumishi.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo walipokea na kupitisha

**_KUMB. NA. KWI/146/2021:_ TAARIFA YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA (UVICO -19) NA UJENZI WA KITUO CHA AFYA**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Ufuatiliaji na Takwimu aliwasilisha taarifa na kueleza kuwa Halmashauri ilipokea fedha kiasi cha Tshs. **480,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba **24** vya madarasa na ofisi **14** za walimu, madarasa 17 kwa shule **11** za Sekondari na madarasa **7** kwa shule shikizi **3**. Aidha aliendelea kueleza kuwa Halmashauri imepokea **Tshs. 250,000,000.00** za tozo kwa ajili ya ujenzi wa jengo la maabara na OPD katika Zahanati ya Rwamlimi. Ujenzi unaendelea na uko katika hatua mbalimbai za ukamilishaji.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo, walijadili na kuipitisha

**KUMB. NA. KWI/147/2021: TAARIFA YA UAMUZI WA WAZAZI KUHUSU UANZISHWAJI WA SHULE YA MFUMO WA KIINGEREZA (MUKENDO)**

Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi aliwasilisha taarifa na kueleza kuwa katika kikao cha wazazi cha tarehe **10/12/2021** kilichohudhuriwa na wazazi **102**, kilijadili na kutoa maamuzi kuwa wanafunzi walioko shule ya Msingi Mukendo wasiondolewe

kwa kuwa wazazi hawako tayari kukubaliana na wazo la kubadili Mukendo kwenda mfumo wa Kiingereza. Aliendelea kueleza kuwa kwa kuwa zoezi hili lilisitisha uandikishaji wa wanafunzi kwa darasa la awali na darasa la kwanza, Menejimenti ilipendekeza uandikishaji uanze ili kuendana na muda.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo, walijadili na kuipitisha.

***KUMB. NA. KWI/148/2021:* MAOMBI YA MABADILIKO YA MATUMIZI YA FEDHA ZA UJENZI WA MADARASA KUTOKA MAPATO YA NDANI PAMOJA NA KUHAMISHA KIFUNGU CHA UJENZI WA SHULE MPYA YA KATA KIGERA**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa na kueleza kuwa Halmashauri ilipokea jumla ya **Tshs. 470,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Kata ya Kigera na eneo lililopendekezwa kujengwa shule hiyo linahitaji kulipiwa fidia ya **Tshs. 82,975,148.00** kwa watu **11**, Menejimenti inaomba ridhaa ya kubadilisha matumizi ya fedha za mapato ya ndani ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu katika shule za Sekondari za Nyamitwebiri, Mshikamano, Nyasho na Mwisenge ziweze kulipa fidia ya eneo hilo na ujenzi uanze, wajumbe waliridhia mabadiliko hayo na kuruhusu taratibu ziendelee. Aidha aliendelea kueleza kuwa Menejimenti inaleta maombi ya kuhamisha kifungu cha ujenzi wa shule mpya ya Kata ya Kigera kiasi cha **Tshs. 470,000,000.00** zilizotolewa na mradi wa SEQUIP na kupokelewa shule ya Sekondari Kiara lakini vifungu vyenye malipo vilikasimiwa kwenye vifungu vya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma Makao Makuu hivyo kushindwa kufanya malipo na kuendelea na ujenzi . Menejimenti inaomba ridhaa ya kuhamisha vifungu hivyo toka ngazi ya Halmashauri kwenda shule ya Sekondari Kiara zilipopokelewa fedha ili kuruhusu malipo kufanyika na ujenzi kuendelea kwa wakati.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuruhusu taratibu ziendelee.

**KUMB. NA. KWI/149/2021: MENGINEYO**

Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika aliwasilisha taarifa juu ya mkutano wa Maafisa Ugani uliofanyika Mkoani Singida na kueleza kuwa kutokana na ukuaji wa teknolojia ufugaji wa nyuki umeboreshwa na kupelekea mazao yatokanayo na nyuki kuwa na kiwango kikubwa cha virutubisho. Menejimenti ilishauri iandaliwe siku rasmi kwa ajili ya mafunzo ya ufugaji wa nyuki na mazao yake. Aidha Menejimenti imeshauri kuwa sehemu ya wanaume ya kujisaidia haja ndogo iko wazi hivyo uwekwe ukuta ili waweze kujistiri wakati wa huduma hiyo

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma alieleza juu ya makabidhiano ya vyumba vya madarasa na taarifa ya kikao cha wazazi wa watoto wa shule ya msingi Mukendo na kueleza kuwa wazo hili lipelekwe kwenye kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala ili zoezi la uandikishaji lianze.

**KUMB. NA. KWI/150/2021: KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kufunga kikao mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa mchango wao wa mawazo baada ya maelezo hayo mwenyekiti alifunga kikao saa **12.20** jioni.

***Muhtasari huu umethibitishwa leo tarehe*** 28/07/2022

***Saini:*** [signature]
***Jina:*** LAZARO N. NAMKALE
***Katibu***

***Saini:*** ____________________
***Jina:*** ____________________
***Mwenyekiti***

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA.

## YATOKANAYO NA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KIKAO CHA KAWAIDA CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO (CMT) KILICHOFANYIKA TAREHE 10/12/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA MANISPAA MUSOMA.

| KUMB. NA. | AGIZO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| KUMB. NA. KWI/143/2021 | i) **Kuhusu hoja ya kupunguza matumizi ya umeme na maji katika majengo ya Halmashauri ya Manispaa.**<br><br>**AZIMIO:**<br>Majengo yote yanayotumia umeme na maji ya Halmashauri ya Manispaa yaainishwe kisha andiko liandaliwe kwenda CMT ili kuona namna bora ya kudhibiti matumizi haya. | **ME** | ▪ Agizo limetekelezwa. Jengo la Canteen (Mama Mariam), Ofisi ya SACCOS na Ofisi za Zimamoto zinatumia umeme wa Manispaa bila kulipa.<br><br>▪ Andiko limeandaliwa. |